

SOKOINE UNIVERSITY OF AGRICULTURE



**OFFICE OF THE DEPUTY VICE CHANCELLOR
(ADMINISTRATION AND FINANCE)**

P.O. BOX 3000, CHUO KIKUU, MOROGORO, TANZANIA
TELEPHONE: +255 023 260 3511-4, Direct +255 023 260 4653,
FAX: +255 023 260 4573.

E-mail: dvadminfin@suanet.ac.tz

Kumb. Na. SUA/ADM/H.1/13

Tarehe: 21.08.2013

Wafanyakazi wote

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo

MOROGORO

YAH: UTEKELEZAJI WA SERA MPYA YA AFYA YA CHUO, 2013

1.0 UTANGULIZI

- 1.1 Katika mkutano wake wa Septemba mwaka 2006 BARAZA la Chuo liliidhinisha Sera ya Afya ya Chuo. Pamoja na mambo mengine Sera hiyo ilianzisha Mfuko wa Afya ya Jumuiya ya Chuo, "SUA Community Health Fund" ambao utekelezaji wake ulianza mwaka 2007.
- 1.2 Kwa mujibu wa Sera ya Afya ya Chuo, 2006 wafanyakazi wote wa Chuo na wanafunzi walitakiwa kuwa wanachama wa Mfuko wa Afya ya Jumuiya ya Chuo.
- 1.3 Sera ya Afya ya Chuo na Mfuko wa Afya wa Jumuiya ya Chuo, vilianzishwa kwa kuzingatia Sera ya Afya ya Taifa ambayo pamoja na mambo mengine inatoa mwongozo wa jumla kuhusu fursa na nafasi ya jamii kuchangia gharama za huduma za Afya (Aya ya 5.4.8.2) ya 1990, kama ilivyohuishwa mwaka 2007.

2.0 SERA YA AFYA YA CHUO, 2013

- 2.1 Katika mkutano wake wa 129 uliofanyika tarehe 27 mwezi Juni, 2013 BARAZA la Chuo liliidhinisha mapitio ya Sera ya Afya ya Chuo ambayo imeanza kutumika tarehe 28 Juni, 2013. Pamoja na mambo mengine yaliyojitokeza katika Sera hiyo badiliko kubwa ni kuruhusu wafanyakazi kuchagua mfuko au bima ya afya ya chaguo lao. Kwa mantiki hiyo wafanyakazi hawalazimishwi kuwa wanachama wa Mfuko wa Afya wa Jumuiya ya SUA ila wanatarajiwa kwa hiari yao wenyewe, kubaini manufaa na kujiunga au kuendelea kuwa wanachama wa "SUA-CHF".
- 2.2 Madhumuni ya waraka huu ni kuwafahamisha wafanyakazi mambo yanayowapasa kuyafahamu kuhusu utaratibu wa utekelezaji wa Sera Mpya ya Afya ya Chuo iliyopitiwa upya hususan kuhusu uchangiaji wa gharama za matibabu kama ifuatavyo:-

